**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**FOMU YA MKATABA WA UJENZI KWA FUNDI**

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

| | | |
|---|---|---|
| 1 | MWAJIRI | Mkuu wa Chuo<br>Chuo cha ualimu wa Ufundi stadi Morogoro.<br>S. L. P 671 Morogoro<br>Kny:<br>Katibu Mkuu<br>Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia<br>PRINCIPAL VOCATIONAL TEACHERS TRAINING COLLEGE P. O. BOX 671 MOROGORO |
| 2 | JINA NA ANWANI YA FUNDI (*Mwajiriwa*) | Jina: ATHUMAN. S. MWANDE<br>Anwani: S.L.P. 400. Kolo Gwe<br>Simu: 0684.192.750 |
| 3 | ENEO LA UJENZI | *MVTTC – MOROGORO* |
| 4 | MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI | *KAZI YA BOMBA KWENYE JENGO LA BWENI WASICHANA (TYPE ONE)* |
| 5 | GHARAMA YA UFUNDI (*+ Skills Development Levy*): | *Tsh. MILIONI SABA NA LAKI NANE (7,800,000)* |
| 6 | MUDA WA MKATABA<br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): | Tarehe ya Kusaini 25/10/2021<br>Muda: siku 120 (*Taja idadi siku*)<br>Tarehe ya Kuanza Kazi 15/12/2021<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi 15/4/2022 |
| 7 | MASHARTI YA MALIPO: | • Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa kwa awamu 5 baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa |

## B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya Mtaalamu Mshauri. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi *(kama inavyooneshwa katika kijeduari hapa chini)* na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.

### 3.1 Jeduari la mchanganuo wa kazi Bomba.

MUAINISHO WA GHARAMA ZA KAZI YA UFUNDI BOMBA JENGO LA BWENI WASICHANA (TYPE ONE)
JINA LA FUNDI Athuman S. Mwande

| MCHANGANUO GHARAMA WA KAZI ZA BOMBA KATIKA JENGO LA WASICHANA | |
|---|---|
| NA KAZI | GHARAMA |
| 1.Kutindua na kuweka bomba za maji safi na maji taka kwenye kuta na sakafu sehemu zitakazohitajika kama inavyoonekana kwenye michoro na maelekezo yatakayotolewa na msimamizi wa kazi. | 1,800,000 |
| 2.Kufitisha vifaa vyote vya maji safi na maji taka mfano masink ya kunawia, tepu za maji n.k kama inavyoonekana kwenye michoro na maelekezo yatakayotolewa na msimamizi wa kazi. Vyooni, bafuni na raundry | 3,500,000 |
| 4.Kujenga chemba zisizopungua arobaini kuunganisha mfumo wa maji taka. | 2,500,000 |
| **JUMLA YA GHARAMA ZA UFUNDI** | **7,800,000** |
| **JUMLA KUU (GHARAMA ZA KAZI+ KODI)** | **7,800,000** |

4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.

7. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.

8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.

10. Ucheleweshaji wa Kazi:

- Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

13. Maelekezo ya kazi yatatolewa na msimamizi mkuu wa kazi (Clerk of works) na mwajiriwa (Fundi) ataomba malipo fedha kwa kazi aliyoifanya kwa mkuu wa Chuo kupitia msimamizi wa kazi na atalipwa endapo ukubwa wa kazi aliyofanya itakaguliwa na kufika angalau 30%.

**MWAJIRI:**

Saini: ..............................

Jina : Ephrem Matambi

Cheo: Kaimu M/Chuo

Tarehe: 30/11/2021

PRINCIPAL
VOCATIONAL TEACHERS TRAINING COLLEGE
P. O. Box 671
MOROGORO

**FUNDI:**

Saini: ..................

Jina: ATHUMAN S. MWANDE

Cheo: FUNDI BOMBA

Tarehe: 25/11/2021

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ..............................

Jina: ANDREW A BOI

Cheo: KAIMU MKUU WA MAFUNZO

Tarehe: 30/11/2021

**SHAHIDI WA FUNDI**

Saini: ..................

Jina: SAIDI SAIDI

Cheo: FUNDI

Tarehe: 25/11/2021